



Kanuni takatifu iliandikwa na Mchungaji Sun Myung Moon huko Korea. Ujumbe wake ulioandikwa kwa lugha ya Kikorea ulitafsiriwa kwa mara ya kwanza kwa Kiingereza na sasa umetafsiriwa kutoka Kiingereza hadi Kiswahili. Kanuni hii takatifu inafungua njia kwa yule anayetafuta majibu ya ukweli kwa maswali mengi ya kimsingi hii si tafsiri rasmi kwa mujibu wa baraza la Kiswahili Bakita na tunaomba kwa unyenyekevu msomaji asiwe mkali hata kidogo katika uwasilishaji na tafsiri, jambo ambalo si la moja kwa moja. kutoka Makao Makuu ya kanisa la umoja, lakini kwa wafuasi rahisi na wa kujitolea wa Baba Moon, wanapotaka kusambaza ujumbe wake kwa watu wanaozungumza Kiswahili. Tunapenda kukualika usome kwa makini kitabu hiki kitakachokupa maono mapya ya ulimwengu. na itabadilisha maisha yako yote.

# SIKU MOJA TUNAPOPOKEA BARAKA

**(A day when we welcome the blessing)**

**September 22, 1978 – Kamikawa, Japan.**

---

Leo tuna sherehe mbili mbele yetu – uchumba na ubadilisho wa uzazi wa damu. Hizi ni sherehe za malipizi kwa kuweka sharti ambalo kwa kupitia kwalo tunaweza kuzaliwa upya kwa Wazazi wa Kweli. Uzao mpya una umuhimu kwa sababu sisi tulizaliwa katika dunia ya kishetani. Mwanamke ndiye aliyeanguka kwanza, basi mwanamke anapaswa kukombolewa kwanza, na halafu mwanaume anapaswa kuzaliwa upya. Kwa kupitia Sherehe ya Divai Takatifu tunapitia utaratibu huu kimoyomoyo. Siku arobaini baada ya Baraka, kunakuwa na sherehe moja ambayo kwayo tunazaliwa upya kwa namna ya nje. Zote ni sherehe za malipizi. Kwa kuzipitia, tunaenda kupita kipeo cha Adamu na Hawa walioanguka hadi kipeo cha ukamilisho kiroho. Baada ya mwanaume na mwanamke kulinda nafasi moja kwa kuongozwa na mbingu, wao wanaweza kuunganisha kipeo hiki cha upendo na upendo kati ya mume na mke, na ndoa yao inawekwa imara.

Siku ingine, nilitoa ufafanuzi ufuatao Uingereza : urembo wa mwanamke hauishii katika sura yake (watu kwa kawaida wanaangalia sura kama kigezo cha uzuri wa mwanamke) Lakini ni sehemu tu ya mwili. Tunapaswa kuangalia kwa ujumla. Sura ni sehemu ya tatu ya kuangalia. Inatupasa kumwona mwanamke kwa mbele, kwa ubavu, na kwa kuzingatia utu mzima, kama vile mikono na miguu yake, namna yake ya kutembea, sauti yake, na vingine vivyo. Kadhalika, sura ya kupendeza ya mwanaume inahusisha mengi zaidi kuliko uso wake. Kwa hivyo, msingesema kwamba uso wa mke wako ni mzuri au mbaya. Wanawake warembo wengi wana akili punguani kwa sifa za roho, na mwanamke wa wema na ajili nzuri anaweza kutokuwa mrembo. Mwanamke ambaye urembo wake unaishia tu na uso wake mara chache unaishia baada ya watoto wawili au watatu. Inapendeza siku zote kuona kama mwanamke huyu anaweza kushika urembo wake baada ya kupata watoto.

Kuna njia mbalimbali za kuchanganua viungo vya mume na mke. Kama vile kila mtu ana uso tofauti, kadhalika, bahati za watu ziko tofauti. Ajali ya kila mtu katika maisha ni tofauti. Kama ajali ya mtu ni mbaya, yeye anaweza kuifidia na ajali nzuri ya mke wake. Kadhalika, kama ajali ya mke ni mbaya, ajali nzuri ya mke wake inaweza kuisawazisha. Kwa hivyo, kuoza mume na mke ni sawa na kuzalisha mahali pa sawa toka mlimani na bondeni. Vitu vingi vinaweza kulimwa juu ya nchi pana nafaka, matunda, mboga na vinginevyo. Hii inatusaidia kuelewa kwamba masuala ya nje mengi ya mume na mke hayahitaji kufaa pamoja mara moja. Uso unavumbua nafsi ya mtu. Ni muhimu kulielewa hilo unapoongoza watu au kuwagawia majukumu. Hata pua na sikio la mtu linaweza kuonyesha nafsi yake yote. Mungu pia aliumba wanyama kwa kulingana na kanuni hii. Mchukue simba, kwa miguu yake ya mbele yaliochongwa vizuri na viungo vilivyowiana. Yeye kwa kweli anastahili kuitwa mfalme wa wanyama. Watu wako hivyo hivyo. Ninapoangalia mkono wa mtu, ninaweza kuelewa mara moja kama ana kipaji katika kazi ya kuchonga au kazi ya kusoma na kuandika vitabu au katika sanaa, kama yeye ana mkono wa wizi. Nikiangalia miguu ya mtu, ninaweza kusema kama anaweza kukimbia kasi au hapana.

Kama masharti ya kiroho katika ndoa sio mazuri, taabu nyingi zinaweza kutokea, kama vile kifo katika ajali ya gari. Kwa hivyo, tafadhali eleweni wazi kwamba sheria zisizoonekana kupitia ufahamu wenu zinatenda kazi. Kwa kuangalia kizazi kimoja peke yake, hamwezi kusema familia itanufaika. Mnahitaji kuchunguza angalau vizazi vitatu, au kwa uhakika zaidi, zaidi ya vizazi saba. Hata ukifikiria kwamba wewe na mwenza wako hamfai kuwa pamoja, tafadhali ishini pamoja kwa angalau miaka mitatu. Tafadhali muwe na uhakika na fanyeni jitihada ya kuungana, kwa kuelewa kwamba mimi nilifuata njia hiyo hiyo.

Mtu wa anguko hakuwahi kamwe hata kuota kubarikiwa chini ya uongozi wa Mungu. Mungu alikuwa akiongoza maongozi yake hadi sasa kwa kupitia dini ili kuipokea siku ile. Mungu alishauri wazo la jamii moja la watu teule ndani ya Waisraeli na aliwafundisha kuhusu Masihi, akipanga kukomboa kwa njia yao

msingi wa ushindi kitaifa. Lakini maongozi yale yalishindwa. Kwa kuwa uhusiano wa imani na upendo ulishindwa kuendelea kati ya viongozi wa Uyahudi na Yesu, Mungu alilazimika kuchagua Wakristo kama chombo chake. Kwa hivyo, Ukristo ulikuwa Israeli ya pili. Wakiwa wamekatiwa baraka na ulinzi maalum unaofuatana na watu teule wa Mungu, Wayahudi walitekwa na shetani, na walitembea njia isio na mwisho kushutumiwa na kumwaga damu.

Kiwango cha dunia cha roho

Katika nyakati za Ujio wa Pili, Israeli na Korea kila moja ilishuhudia uhuru wake kwa wakati mmoja. Israeli, taifa dogo mno kiasi hicho, ilipambana na mataifa ya Kiarabu na kuyashinda. Kwa kuwa huu ni muda wa Ujio wa Pili, Israeli inaweza kubarikiwa. Tangu miaka elfu mbili, Uyahudi ilisimama katika nafasi ya kutimiza kazi kuu kwa dunia; kulikuwa na jamii nyingi za Wayahudi katika himaya ya Warumi. Ingawa, kwa sababu Yesu alisulubishwa,

sio Uyahudi tu, na Ukristo vile vile, ulipoteza msingi wa kupata ushindi duniani. Historia ya wote Wayahudi na Wakristo kwa miaka 2000 iliyopita ilitiwa mawaa kwa damu, walivyotamani kufungua Ufalme wa Mbinguni wa kiroho. Israeli ilimwaga damu yake kwa namna ya nje na Ukristo ulimwaga damu yake kwa namna ya ndani. Pamoja walikuwa wanaweka njia hii kimwili na kiroho.

Katika muda huu wa Ujio wa Pili, inatubidi kuimarisha msingi huu wa kiroho katika msingi wa kimwili – kwa jina, Ukristo hauna budi kumuamini Bwana wa Ujio wa Pili. Kanisa la Umoja liliongoza njia hii kwa kutangaza kwamba Ujio wa Pili u mikononi. Baada ya ukombozi wa Korea katika mwaka 1945, Kanisa la Umoja lilipoanza, kama Ukristo madhubuti, chini ya uongozi wa makanisa ya Korea, yangeungana na sisi na kutupokea, dunia ya kidemokrasia ingelindwa, na isingekuwa kamwe jamii iliyogawanyika, fisadi ilivyo leo. Juu ya hayo, ujamaa ungepotea juu ya uso wa dunia. Ila, upinzani toka makanisa madhubuti ulifunga njia yetu. Ukristo uliendelea toka kiwango cha mtu peke yake hadi kiwango cha ukoo, kabila, taifa na dunia. Kwa wakati huu wa maana katika maongozi, msingi wa kiroho wa Ukristo ungeweza kuunganishwa na msingi wa kimwili duniani, kwa kuongozwa na Shirika la Umoja, katika muda wa miaka saba. Tulishirikiana na watu toka vyeo vya juu vya makanisa ya Kikristo kwa kusudi hili. Kazi yangu baada ya ukombozi wa Korea mwaka 1945 ilikuwa kuhitimisha maongozi haya kwa kuunganisha makanisa yote kwa kuzingatia malengo ya Shirika la Umoja.

Lakini nilipingwa vikali. Basi msingi wa kiroho wote wa Ukristo ulipotezwa katika maongozi. Kwa hivyo, ilinibidi kuanza bila msingi wa kimwili. Niliachiwa katika ghorofa ya chini kabisa ya maongozi. Masharti yote yaliowekwa katika historia ya maongozi ya miaka 6000 yalifutwa. Siwezi kusema kwamba nilikamilisha utume wangu duniani hadi nitaweka sharti kwa ajili ya upeo wa roho na maadili kuenea kote chini ya uongozi wa nchi ya Korea.

Kwa hivyo, ili kuweka msingi huu, nilikuwa naweka njia na kutanua Shirika hili bila neno moja la nung'uniko, kwa kupokea na kusharabu shutuma hadi miaka ya 1970. Inatupasa kukomaa kiasi cha kwamba tunaweza kukamilisha upeo wa ushindi kiroho na kimwili kwa shughuli ya Shirika la Umoja pekee, katika tukio hakuna awezaye kutusaidia. Kwa kufanya hivi, hatuwezi kuishi kwa ajili ya Shirika la Umoja tu. Utume wa Shirika la Umoja na kuweka upeo wa maadili kwa taifa moja kabla ya kuendelea na kiwango cha dunia nzima. Hatuna budi kuweka hata kama Shirika lenyewe linasulubishwa kwa kufanya hivyo.

Hilo lilikuwa mwelekeo wetu katika miaka ya 1970 – wakati wa ndoa ya wabarikiwa 777. Ninafikiri mnaelewa kwamba maongozi ya kimbingu, kwanza kutimiza upeo wa roho kifamilia na kisha upeo wa maadili kitaifa. Kwa kusudi hili, tulikuwa tunatunga familia tangu miaka 1960. Kulikuwa na Baraka za familia 36, familia 72, familia 124, familia 430, na familia 777. Familia hizi zote zinadhaniwa kujenga msingi wa ushindi kama familia zilizokombolewa kwa masharti juu ya kiwango cha dunia nzima. Nilikamilisha msingi wa ushindi juu ya kiwango cha taifa. Halafu ilinibidi kuanza njia yangu kwenda mbele kwa ukombozi wa kiwango cha dunia.

Hata kama nilifanya msingi wa ushindi huko Korea, kwa kuwa msingi wa Ukristo uko katika kiwango cha dunia nzima, sina budi kuwafikia Wakristo wa dunia. Ukristo madhubuti wa Korea ulinipinga, ila Uingereza na Amerika hawakunipinga kwa wakati ule wa maana. Hasa, Ukristo wa Magharibi ulishindwa kuingilia kwa kutawanya shutuma, ila hawakunipinga moja kwa moja. Sababu nilijia toka Amerika ilikuwa kuweka huru ulimwengu wa Ukristo wa Amerika ili ingeweza kutumiwa zaidi moja kwa moja na Mungu katika maongozi ya leo. Amerika, niliweka msingi wa ushindi juu ya kiwango cha taifa katika miaka mitatu – 1972, 1973 na 1974. Kwa wakati ule, nilipokelewa kwa shangwe katika miji yote ya Amerika niliyoitembelea. Uma kwa ujumla ulinipokea, ingawa jamii ya Wakristo wote halali haikutupokea. Wavumi wa kale na Uyahudi halali waliungana katika kumpinga Yesu, lakini sasa hali ni tofauti. Uma kwa ujumla ulinipokea. Ukristo ulitupinga tu kama kundi ndani ya jamii kwa ujumla. Kwa hivyo, nilipata ushindi mkubwa iwayo yote.

Juu ya msingi wa bahati njema hii, nilianzisha Pigano la Kimataifa la Dunia Moja (PKDM) =[International One World Crusade (IOWC)] kwa kuleta waumini toka pande zote za dunia kwenda Korea. Kwa nini nilifanya hivi ? Upeo wa wokovu kiroho tayari ulishaumbwa upya kwa njia ya mapokezi mazuri na watu wa Amerika, ila ilitakiwa kuunganishwa na upeo wa kimwili: watu walitakiwa kuvutiwa kuungana na sisi katika kufuatilia lengo letu la kukomboa dunia. Kampeni ya PKDM=IOWC katika mwaka 1975 ilianzishwa kwa kuwa na dhumuni hili akilini. Kwa kuongozwa na IOWC, tulishughulika kwa kuweka Shirika la Amerika katika shauri ya kimwili. Ingawa Shetani alikabiliana na sisi, sikupondwa katika vita ile na sikurudi hapa mshindwa. Badala, nilirudi mshindi

kabisa.

Historia ya maongozi kwa mara nyingi ilirefushwa. Maongozi ya Mungu ni kutimiza kusudi la ukombozi chini ya uongozi wa familia; inakusudia kuanzisha mahusiano kamilifu ya aina ya familia juu ya viwango vyote toka mtu binafsi hadi dunia. Sasa Shirika la Umoja kwa uthabiti linasonga mbele kuelekea ukombozi wa familia juu ya kiwango cha dunia.

Msingi wa Baraka

Mambo haya yote yanatusaidia kuelewa kazi ya taabu na kujitoa mhanga kwa Mungu katika historia kwa ajili ya kuipokea siku hii, mtu wa dhambi anapoweza kupokea Baraka. Tokea zamani kwa kupitia maelfu ya miaka, watu wengi mno walianguka kando ya njia, na ndani ya familia, jamii, makabila na mataifa, mabilioni ya sadaka yalitolewa. Ila, hakuna hata mmoja aliyeweza kupokea Baraka chini ya uongozi wa Mungu. Shirika la Umoja ilibidi lifikie kiwango cha dunia nzima huko Japan na Amerika baada ya mapigano mengi. Sasa tumeingia ndani ya ulimwengu wa kihistoria, wa ushindi.

Kabla ya nyie kupokea Baraka, mnapaswa kuona maana halisi ya kihistoria ya maisha yenu. Maongozi ya Mungu yalipitia historia ya kujitoa mhanga kwa maelfu ya miaka ili kuleta wokovu. Katika maongozi ya Mungu kulikuwa na manabii wengi, waanzilishi, na watu wa dini wengi ambao walifanya matoleo mengi mno. Wote baina yao walikuwa onyesho la upendo wa Mungu kwenu ili kuwaacheni mkisimama kama mshindi leo. Historia ya Kanisa la Umoja ilikuwa hivyo hivyo. Sababu iliyonifanya kufanya kazi kwa bidii kiasi hicho ilikuwa kufungua njia ya Baraka kwa watu wote, na hata kuongoza njia ya wokovu kamilifu. Mungu alishughulika bila kuchoka kwa ajili ya kila mmoja wetu. Ingetupasa kujisikia shukrani kubwa mno ! Hata kama tunatoa maisha yetu yote, hatuwezi kamwe kulipia madeni yote tunayodaiwa na Mungu.

Lakini kama tunatoa kila kitu, Mungu atatupokea kama washindi kati ya dunia ya kiroho ya milele, dunia ya utukufu. Hii ni jambo la kuogofya. Basi mfahamu ya kwamba nyinyi ni wale ambao mnabeba jukumu la kihistoria kama hili. Nyie mnaitwa kwa kuokoa mabilioni 4 za watu duniani leo kwa uwezo wenu wenyewe. Ili mchukue nafasi yenye madaraka kama hii, Mungu alifanya matoleo, na kila dini ilikuwa inafanya kazi kwa bidii. Ingawa kujitoa huko mhanga kihistoria kutazawadiwa kama tunakumbatia na kukamilisha wajibu wetu kwa imani. Mnalazimika kuelewa wazi kwamba mna utume kama huu. Kwa hivyo, kama mtalonge historia itajongea mbele, Japan itajongea mbele, na dunia itajongea mbele vile vile.

Kuna kitu kingine cha kujali. Kwa sababu Adam na Hawa walianguka, walianzisha masharti yaliyowasababisha wazao wao kumwaga damu na kuchukua historia duni. Ila nyie mnapaswa kuwa tofauti. Chochote mnachokifanya,

msiachie kamwe wazao wenu dhambi. Afadhali, mngewaacha na kipimo kingine cha wema. Haidhuru magumu yote mnayoweza kuvumilia maishani mwenu, jaribu kuenda mbeleni kwa kushukuru. Kuweka moyoni wasiwasi na manung'uniko ni jambo zito. Mna kazi moja ya kuweka huru nyakati tatu – zamani, sasa, na ujao. Mnapaswa kuachia desturi ya ushindi kweli kweli ili wazao wenu wasirithi desturi ya malipizi. Nafasi ya kubarikiwa ina maana halisi kubwa zaidi. Jamii ya binadamu nzima, ya zamani na ya sasa, itakuja kututegemea sisi. Ni jambo la thamani kubwa kupita maneno kwamba Masihi amekuja tena na ameimarisha nafasi ya bibi arusi na bwana arusi kwa ajili ya kutoa Baraka.

Wajibu wa mtoto wa baba mkubwa ni kurithi kila kitu toka kwake. Wote wanasimama juu ya chimbuko kuu moja, lakini upeo wa maisha yao ni tofauti. Ncha kuu ambapo ninasimamia na ncha ambapo nyie wana ndoa wa kubarikiwa mtasimamia ni moja. Hakuna ncha mbili. Tafadhali mlielewe hili. Mimi nina kazi ya kiwango cha dunia na nyinyi mna kazi ya kiwango cha mtu binafsi – ila unaweza kutanua upeo wako kwa uhuru kwa kushindana juu ya kiwango cha ukoo, kiwango cha kabila na viwango vya taifa au vya juu zaidi. Msijiwekee kamwe mipaka kwa sababu ya nyinyi kuwa Wa-Japan. Kiini ni kile kile na kanuni kwa kufanikiwa ni ile ile, kwa yote maisha yangu kifamilia na maisha yenu ya kifamilia, katika maisha ya kiwango cha ukoo wangu na maisha ya kiwango cha ukoo wenu, na desturi mbalimbali za maisha juu ya viwango vya kabila, taifa, dunia na ulimwengu. Tofauti moja tu ni kwamba mnapaswa kuwa Masihi wa ukoo. Ningeongea na nafasi hii kuhusu Home Church (=Kanisa la nyumbani), lakini sina muda kwa ajili ya hili sasa.

Bado sijakamilisha ulimwengu wa ushindi na kiwango cha dunia. Bado ninapigana na kutumia maarifa mbalimbali ya kivita kwa wakati huu. Mnapofikia kiwango cha dunia, mnaweza kufanya kila kitu kwa namna kubwa zaidi, basi tafadhali mjifunze kufanya mambo kwa bidii sana pale mlipo sasa. Tafadhali mfahamu kwamba hii ni nafasi mtakuwa nayo baadaye. Je mnaelewa ? Kumbukeni jinsi gani wajibu wenu ulivyo mgumu. Kama mnaweka msingi

wa Ufalme wa Mbinguni na kujenga nguzo za Hekalu la wema wa dunia. Je nyinyi ni nguzo za aina bora ? Je zinaweza kuwa nguzo ambazo zinaimarisha upeo wa wema ? Kama sio, hamna muda wa kuzidi kuchukua mapumziko au kujiingiza katika majadiliano au kuamrisha wengine kwa nguvu.

Mume anazaliwa kwa ajili ya mke, na mke anazaliwa kwa ajili ya mume. Kama mnajidai nafsini mwenu, Mungu anaacha ndoa yenu; kama unamheshimu mwenza wako, Mungu ataingia ndani. Mume na Mke watembee pamoja kama vile miguu miwili katika upatano, kwa kusawazishana wao kwa wao, sio kama mguu mmoja usio imara.

Je mlielewa upeo unaotakiwa kwa Baraka ? Daraja lenu na langu kwa uhusiano wa upeo ule hayako sawa. Nyie hamsimami bado juu ya upeo ule pia hamjapokea

urithi wa kiwango cha familia. Mnatakiwa kufanya nini ili kusimama katika daraja lile ? Mnapaswa kushinda juu ya Shetani. Je mmeshinda juu ya Shetani ? Kama Japan yote itawapingeni, ninafikiri wengi baina yenu watakimbia.

Mbele ya upendo wa Mungu, hatuna budi kutobadilika kabisa. Mungu ni yule aliye wa pekee, yakinifu, na daima. Wale ambao wanaongea juu ya ulimwengu wa roho ya Mungu, kama tunavyofanya, hawana budi kusimama juu ya daraja la roho kama hili. Wale wanaojiunga na Shirika la Umoja na baadaye wanaondoka na kurudi kwa nia zao sio waaminifu. Ni tunapotafuta tu ulimwengu wa upendo wa Mungu ambao kabisa haubadiliki, usiogeuka daima ndipo yeye anaanza kuishi na sisi. Kwa kufanya hivi, inatubidi kuendeleza nafsi isiobadilika na ya daima ambayo inaweza kumshinda Shetani. Hamjasimama katika nafasi ile bado. Kwa kutimiza hili mnapaswa kurithi upeo wa ushindi wangu.

Sherehe ya Uchumba

Katika Japan, kuna majengo makubwa mno. Mtu ambaye jina lake linaonekana juu ya hati ya kumiliki anamiliki jengo. Mnaweza kuwa mmilikaji wa jengo kwa kipande cha karatasi tu. Kwenu nyie kurithi kila kitu toka kwangu ni sawa. Mimi natimiza ushindi wote wa ukombozi wa ulimwengu na kujenga jengo nzuri sana kwa kiwango cha dunia, kuandika hati za umilikaji zote, na halafu kuzihamisha kwenu kwa njia ya Baraka. Ni rahisi, au sio ? Nyie wote hapa ni wamilikaji wa jengo nililojenga. Nafasi yenu inakuja tu kama vile. Inakuwa kama vile nyie wote mnasimama sasa katika mstari wa kuanzia; juu ya uwanja wa mashindano ya ustadi wa michezo. Mjaribu kukimbia mbio kwa nguvu mwezavyo. Kwa hakika kabila kiongozi la Japan litachipuka toka kwenu. Kwa uwezo wetu sisi wenyewe hatuna thamani; tunahubiri tu, na tunajaribu kuishi kikanuni. Kwa sababu ya urithi wetu, Shetani hawezi kufanya chochote. Leo, tutapitia sherehe ya kuhamisha “hati za kumiliki” kwa kulingana na Kanuni.

Tunapokea Baraka juu ya ahadi ya kwamba tutailinda na kuiacha kama hazina kwa uzao wetu hadi maelfu ya vizazi. Kama mtaiharibu, ukoo wenu utakuwa katika matatizo. Kwa hivyo, jambo la msingi ni jinsi gani kuendeleza uzazi wa damu safi ambao mbingu inatukabidhi sasa. Kwa kufanya hivi, inatupasa kuishi kwa unyofu wa moyo. Adamu na Hawa walianguka katikati ya Bustani ya Edeni safi; basi, swali la muhimu sana ni jinsi gani kujiweka sisi wenyewe safi katika dunia hii ya dhambi. Tunakabiliana na matatizo makubwa mno, hata tukifanya kazi kwa nguvu na kujitolea sisi wenyewe. Kwa haraka tunapaswa kuandaa mazingira ya watu wote ili wale watoto wabarikiwe wanaokuja wasinajisiwe. Huu ndio wasiwasi wangu, na inatupasa kuharakisha.

Kuna kuwa na sherehe mbili ambazo kwazo tunarithi uzazi wa damu safi. Ya kwanza ni Sherehe ya Uchumba. Kwa nini tunakuwa na Sherehe ya Uchumba ? Adamu na Hawa katika Bustani ya Edeni walikuwa katika kipindi cha uchumba.

Leo, uzao wa dhambi umeongezeka na kujaza dunia. Baraka inafanyika katika mazingira kama hayo. Macho yetu yanahangaishwa na wanaume na wanawake wengi mno duniani. Bustani ya Edeni ilikuwa na Adamu na malaika mkuu tu ndani yake. Malaika mkuu alianguka na kuwa Shetani. Kwa hivyo, inatubidi kutwaa ushindi juu ya Shetani. Lakini kutwaa ushindi kama huo, inatupasa kujua yeye ni kiumbe wa aina gani ? Shetani alishindwa kuungana na Mungu, na badala yake aliteketeza upendo kwa kujiweka mwenyewe katikati. Lakini sisi tuko tofauti. Tunatenda upendo kwa kuongozwa na Mungu.

Wanaume na Wanawake wote katika dunia ya kiulimwengu wako katika nafasi ya Adamu na Hawa walioanguka, wavulana na wasichana wa Shetani. Kwa hivyo, tatizo ni jinsi gani kubadili wanaume na wanawake kama hawa kuwa vijana na mabinti wa Mungu. Inafanyika kwa Kanuni, ambayo inafundisha kwamba Adamu mkamilifu anapofika, Hawa mkamilifu anakombolewa. Chanya (+) kamilifu anapotokea, hasi (-) kamilifu bila shaka

anajidhihirisha mwenyewe. Hii ni Kanuni ya uumbaji. Mtu mmoja anapokuwa hasi (-) kamilifu, chanya (+) kamilifu itatokea. Tambueni kwamba idadi ya watu wanaume na wanawake katika jamii ya binadamu iko karibu sawa. Busara ya mbingu na nchi iliamuru. Kadhalika, upepo unazunguka kwa uhuru, kwa ajili ya kudumisha usawa wa hewa. Mwanaume mkamilifu anapozaliwa, mwanamke mkamilifu anadhaniwa kuzaliwa. Biblia inaposema kwamba mwanamke aliumbwa toka Adamu, ni kwa alama ya jambo hili.

Nyinyi ni Adamu na Hawa walioanguka. Kwa sababu ya anguko, mnasogea mbele kuelekea milki ya ukamilifu kutoka hali ya masharti ya dhambi. Hakuna njia ya kushinda ulimwengu wa malipizi ila kwa kupitia Adamu aliekamilika. Hii ni Kanuni. Adamu mkamilifu huyu anapaswa kuwa mtendewa wa hakika wa upendo wa Mungu. Yeye hana budi kusimama juu ya upeo ule. Bwana wa Ujio wa Pili anakuja kwa ajili ya kutimiza nafasi hii, basi yeye ndiye Adamu mkamilifu. Yeye anakuja kama sumaku kwa kuvuta watu wote, kwa kuongozwa na upendo. Sumaku hasi (-) inavutwa na sumaku chanya (+), hata kama mtu mmoja anaomba isimame. Sumaku hasi (-) ina nguvu ya kuvuta sumaku chanya (+).

Kanuni ya ukombozi iko sawa. Adamu na Hawa walianguka baada ya uchumba wao. Kwa hivyo baada ya uchumba, watu wanapaswa kupita kidahili maongozi ya ukombozi. Tunafanya Sherehe ya Divai Takatifu kwa kumfanya mwanaume mkamilifu kwa njia ya mwanamke ambaye alishazaliwa upya kama hasi (-) kamilifu, au Hawa mkamilifu. Sherehe ya Divai Takatifu inaweka sharti kwa ukombozi wa kiroho. Mwanamke anazaliwa upya kiroho na halafu Adamu anazaliwa upya kiroho kwa njia yake. Siku arobaini baada ya Baraka kunakuwa na Sherehe ya malipizi kwa ajili ya ukombozi timilifu ambayo kwa kawaida inachukua siku tatu. Siku arobaini ni wakati wa malipizi kihistoria. Katika vipindi, mwanzo na ukuaji watu hawana mamlaka ya kufanya ukombozi kwa kuongozwa na upendo. Ni baada tu ya kuingia ndani ya kipindi cha ukamilisho ndipo

inawezekana. Kwa hivyo, muhula wa Adamu na ufuatao ni muda wa mapungufu. Kama tukio, watu hawakuweza kurithi kabisa ulimwengu wa upendo wa Mungu juu ya kiwango cha mwanzo (Wakati wa Agano la Kale) au hatua ya ukuaji kwa kuongozwa na Yesu. Lakini kwa kurithi tu ulimwengu wa upendo wa Mungu na viwango vya mwanzo na ukuaji watu wataweza kuingia katika ulimwengu wa Wakati wa Agano Kamilifu. Sherehe ya Malipizi ina maana halisi kiishara ya kukamilisha urithi huu. Siku ya kwanza ni ya kukomboa Wakati wa Agano la Kale, au Adamu alieanguka. Siku ya pili ni kutimiza utume wa Yesu na kukomboa Wakati wa Agano Jipya. Katika Wakati wa Agano Kamilifu, inayowakilishwa na siku ya tatu, mume anasimama kama bwana arusi katika nafasi ya Yesu na anaimba upya bibi arusi. Basi, kwa mara ya kwanza, yeye anaweza kujihisi nafasi halisi yake kama Adamu aliekombolewa. Ukombozi unataka masharti ya malipizi ya kuonekana na dhahiri.

Sherehe ya Divai Takatifu

Yesu alisema juu ya mkate na divai, “Huu ni mwili wangu…. Hii ni damu yangu…” Divai takatifu ina maana inayolingana. Kwa kupitia Sherehe ya Divai Takatifu tunaweka sharti ambalo kwayo tunapata kuwa wamoja na Wazazi wa Kweli. Mtu ambaye anapata kuwa mmoja wa Wazazi wa Kweli hawezi kuwa mmoja wa Shetani. Daima, yeye amekatwa kwa shetani. Kuanzia sasa, mnapaswa kuwa na uamuzi wa kujenga Ufalme wa Mbinguni mkamilifu mpya kama ma-Adamu na Hawa waliokombolewa katika Bustani ya Edeni ya milele.

Kwa nini tunafanya Sherehe ya Divai Takatifu ? Adamu na Hawa walikuwa wanaishi katika kipindi cha uchumba kabla ya kuanguka kwao. Basi hatuna budi kukomboa kpindi hicho bila uwezekano wowote wa Suto toka kwa Shetani. Kama Adamu na Hawa wangebarikiwa katika ndoa na Mungu na wangependana, kusudi la Mungu lingekamilika. Lakini hawakuweza kulitimiza. Utaratibu wa upendo ulipinduliwa, watu walipoanza kujipenda wenyewe kuliko Mungu au wao kwa wao. Hii inapaswa kusahihishwa. Hii inaitwa ubadilisho wa uzazi wa damu, au sherehe ya upinduzi wa utawala wa Adamu. Hawa alimpoteza Adamu kwa anguko; kwa hiyo, yeye hawezi kupata tena mweza mtarajiwa wake mbele za Mungu isipokuwa yeye kwa unyenyekevu anamweka Adamu katika nafasi ya mzazi. Halafu Mungu anaweza kumfanya kuwa mume wake. Mpaka sasa wanawake waliteswa na kuvumilia mengi katika historia. Wanawake wa Japan, sana sana, walikuwa na historia duni. Wanawake wote walikuwa nyara za wanaume, ambaye baada ya anguko walichukua nafasi za malaika wakuu walioanguka. Tunaenda kulikomboa hili.

Divai Takatifu ni nini ? Inakuwa na mgawo wa vitu vyote ambavyo haviwezi kusutwa na Shetani. Kama mtu aliepokea Divai Takatifu hii na alikuwa mmoja wa

Wazazi wa Kweli analinajisi, ni jambo la huzuni sana. Hali yake inakuwa mbaya sana kuliko shetani. Shetani alinajisi na kuharibu hatua ya ukamilisho ya kipindi cha ukuzi, lakini itawezekanaje mtu mbarikiwa asiwe muaminifu kusamehewa, wakati yeye aliharibu sio hatua ya ukamilisho tu ila tena mwili wa Mungu ? Ni jambo la kutisha.

Mnaweza kuwa hamkujua hili, lakini sasa mnaweza kuelewa wazi kwa kusikiliza ufafanuzi wa Kikanuni huu. Kuanguka ni jambo zito sana. Baada ya sisi kumaliza upito wa tatu wa miaka saba, hii itakuwa kali kweli. Vita yetu ni dhidi ya usaliti wa upendo. Kama mnakosa imani ya kuwa mkweli kwa mweza mtarajiwa wako ni bora zaidi msishiriki katika sherehe hii. Kwa kuwa Kanuni inatatua mambo Shetani ameshindwa kabisa kwangu. Mtu aliegundua siri ya historia na anasimama juu ya msingi wa ushindi wa kweli wa ukombozi wa dunia ni mwiba ndani ya ubavu wa dunia ya kishetani.

Kwa miaka mingi Shetani alinijaribu katika njia aitakayo. Yeye alinijaribu kwa njia nyingi mno ili kunidhoofisha. Kweli sikuanzisha vita kamwe hadi mwaka 1976. Katika mwaka ule, kwa mara ya kwanza, nilifanya mwanzo mpya. Kwa tangazo la mwanzo huu mpya, muda ulibadilishwa. Hadi sasa, maarifa ya vita yetu ilikuwa ya kulinda. Lakini tumeingia katika muda ambapo Kaini analipa malipizi kwa ajili ya Abeli, kwa kuacha nyuma wakati ambapo Abeli analipa malipizi kwa ajili ya Kaini. Ukombozi utaenda mbio zaidi kuanzia sasa. Zamani, Shetani alighafilisha watu wema na kuwapeleka ndani ya Jehanamu. Kuanzia sasa, tutakomboa wale walioangamizwa na kuwaingiza ndani ya Ufalme wa Mbinguni. Njia yetu iko wazi. Tunasonga mbele kwenye Ufalme wa Mbinguni. Kuna kuwa na viwango mbalimbali njiani : viwango vya mtu binafsi, familia, ukoo, kabila, taifa, dunia na ulimwengu. Kila kiwango kwa zamu yake kinapaswa kutolewa kwa ajili ya kufikia kiwango kifuatacho. Mwisho inatupasa kushinda kiwango cha roho ya Mungu hata kama itatubidi kutoa mhanga kiwango cha ulimwengu. Roho ya Mungu ndicho kiwango cha milele ambamo kila kitu kinakamilika. Kila kitu kinafuata Kanuni hii.

Ninajua vizuri sana jinsi gani ukombozi ulikuwa mgumu. Ninapofikiri jinsi gani ilikuwa hafifu na lemevu, siwezi kushindwa hata kama niliamrishwa kufanya vile. Mnaweza kuwaza kwamba Baraka ni kitu rahisi, kwamba mnaistahili baada ya miaka miwili au mitatu, lakini sio kamwe jambo rahisi kama hivyo.

Ninawatakieni nyie wabarikiwa 1610 kuwa familia ambazo Mungu anaweza kustaajabia, kwa kuishi maisha safi kwa nguvu zenu zote. Kubarikiwa ni jambo la maana. Kwa kutazamiwa toka historia ya maongozi, wazo kuu la Mungu ni kujenga upya familia safi, bila hatia ya Adamu na Hawa. Familia ile itakuwa mfano.

Katika utengenezaji (utendaji), mara tu kiolezo kinatengenezwa maelfu au mamilioni zaidi yanaweza kutengeneza. Nilikuwa nikifanya kazi kwa nguvu

kubwa mno hadi sasa ili kuunda kiolezo kile. Kiini cha maongozi ya Mungu ni familia ya Masihi, familia ya Adamu na Hawa waliokombolewa, familia yenye ushindi kupita milki ya anguko. Mtazamo mkuu wa mtu ni kushinda milki ya anguko, na kuunda familia inayoongozwa na upendo, ndani ya milki ya ushindi wa kimbingu. Basi ncha ya Mungu na mtu ni kweli sawa. Mlizaliwa katika upito wa historia ya anguko, lakini mmefikia lengo la walimwengu. Jinsi gani inakuwa ya thamani bora sana ! Kamwe kabla haijakamilika ! Baraka kama hii inasimama juu ya msingi wa yaliyomo wazi ya shauri la ukombozi. Tumeingia ndani ya wakati wa ajabu. Kwa hivyo tunapaswa kufikiri juu ya asili ya familia kwa njia mpya. Familia ya Suzuki, kwa mfano, sio tu familia ya karibu ya mtu mmoja, Mr. Suzuki; ni kiini cha uzao kihistoria ambao unaweza kudumu kwa maelfu ya miaka.

Msingi wa kiwango cha ukoo
Ukamilifu wa familia ya Adamu ulikuwa uwe mwanzo wa ukamilifu wa ukoo, jamii, na taifa na awali ya Ufalme wa Mbinguni. Mnakaribia kiwango ambacho juu yake mnaweza kutimiza utume wenu wa kiwango cha ukoo chini ya uongozi wa familia yenu. Mimi nina utume wa kiwango cha dunia, lakini ncha kuu ambamo tunasimama ni moja.

Yesu hakumaliza kiwango cha msingi wa ukoo; kwa hivyo, yeye hakuoa. Mnapaswa kuelewa hili wazi. Kama utume wa Yesu ulianzishwa kwa kufaulu chini ya uongozi wa familia ya Yohana Mbatizaji, kwa kujenga msingi wa kiwango cha ukoo, Ufalme wa Mbinguni ungeweza kuanzishwa, hata kama Yesu hakushuhudia na alifanya tu kazi ya useremala. Aliyotakiwa kweli kuyafanya ni kuunda msingi wa nafasi nne wa kifamilia kwa kuzaa watoto.

Kwa kusudi lile, Yesu hakuhitaji kujiamini mwenyewe kugeuzageuza makundi na kujiweka hatarini kwa udhalimu. Kama yeye alijenga kwa taratibu masharti ya kulipizia historia ya maongozi, kwa kuongoza msingi wa nafasi wa

nne, maisha yake yasingekuwa yenye taabu kiasi hicho na kifo chake sio cha wakati wake hivyo. Yeye angetuliza kutimiza masharti yale hatua kwa hatua, taratibu ila kwa hakika kwa kujenga msingi wake. Kama angeunda msingi wa familia na angezaa watoto, Ukristo ungekuwa kwa mbali tofauti. Dunia ingevutwa chini ya uongozi wa Yesu kwa kuongozwa na uzao wake moja kwa moja. Lakini msingi hii yote kamwe haikukamilika. Yesu alikufa bila kuwa na msingi wa kifamilia wa kiwango cha ukoo. Kwa sababu hiyo, sisi tunapaswa kuukomboa kwa kulipia malipizi kwa kuhatarisha maisha yetu. Hii ni njia ya Shirika la Umoja, ambalo linatangaza njia ya wokovu kwa watu wote. Upito wa miaka mitatu na upito wa miaka saba ni kiwango hadi ukamilifu wa Ufalme wa Mbinguni duniani. Nyinyi hamwezi kupuuzia mwisho huu. Mna upito wa miaka mitatu kabla ya ndoa na miaka saba baada ya ndoa. Yesu alitakiwa kujenga familia yake katika upito wa miaka mitatu na kukamilisha upito wake wa miaka saba. Kwa hali yetu, tunakomboa wafuasi watatu na halafu 12 katika miaka mitatu; halafu kuwabariki na kutembea upito wa miaka saba. Huu ni mtazamo wa Kanuni. Yesu

alitaka kujenga msingi ambao juu yake angeweza kutanua utume wake kwa kupitia taifa la Israeli hadi dunia. Tunapaswa kukumbatia mambo yote ambayo Yesu hakukamilisha na kuyakomboa kwa kulipia malipizi. Huu ni utume wetu, sehemu ya jukumu letu la asili mia 5, ambayo kwa alama inazingatia historia yote.

Chini ya uongozi wa miaka saba ijayo, mngeshuhudia kwa kufaulu watu 84, mtu mmoja kwa mwezi. Hii ni sehemu ya ulimwengu wa kiwango cha ukoo chini ya uongozi wa watume 12 na wafuasi 72. Wazee wa kabila 72 ni viongozi wa kabila. Kama mnakamilisha hili mnaweza kupata watume 12 kwa kiwango cha ukoo, watatu baina yao wakiwa msingi wa kiwango cha familia. Utume wetu bado ni kujenga msingi wa uthabiti kwa kufanya kazi kwa jasho na machozi, kiroho na kimwili, katika nafasi ya Yesu, hata kama tunasulubishwa kweli kwa kiwango cha familia. Kwa hivyo, ndani ya Kanisa la Umoja, hata kama tumeshafunga ndoa, bado tunazidi kwenda njia ya msalaba juu ya kiwango cha familia ili kutimiza utume huu. Je mnalielewa hili ? Yesu alifufuliwa baada ya kusulubiwa na alikusanya wafuasi wa kufanya chimbuko la kiroho kwa kuongozwa na mitume 12 na wafuasi 72.

Kama hatutakamilisha msingi kama huu wakati bado tuko juu ya dunia hii, daraja linalotuunganisha na Ufalme wa Mbinguni litayeyuka, na tutatakiwa kupambana kwa bidii kwa kulipata tena. Hii ni maana ya upito wa miaka saba. Tunapaswa kushuhudia kwa mtu mmoja kwa mwezi – watu 84 kwa ujumla. Huu ni utaratibu. Mimi sipekui mahesabu ovyo ovyo tu.

Lengo la kwanza ni wafuasi watatu. Katika ukombozi wa familia ya Adamu, watu wanane wanafanya familia moja. Ili kulinda familia ile inatubidi kuwa na wanandugu 12 wanaowakilisha watoto 12 wa Yakobo. Wanakuwa msingi wa ukoo. Ukoo huo unapanuka na kuwa msingi wa kabila. Viongozi wa kuongoza msingi wa kikabila lile ni wazee 72. Kama wangechukua jukumu la kuongoza watu chini ya uongozi wa Yesu, yeye asingesulubishwa kamwe. Upungufu huu bado unabakia katika njia ya ukombozi. Mimi mwenyewe nilifuata utaratibu huu, kwa kubariki familia tatu, halafu familia 36 (ambazo kweli zinawakilisha mihula mitatu ikiwa na familia 12 katika kila muhula), wakifuatwa na 72, 124, 430, 777 na 1800. Kwa kuwa tatu mara sita ni 18, Baraka ya wanandoa 1800 inaweka sharti ya kushinda ulimwengu wa Shetani, kwenda kupita mfiko (uwezo) wake.

Mnapaswa kufuata njia hii kabisa. Kama hatutawajibika kwa dhambi za dunia na kuyalipia malipizi kwa kiwango cha dunia, msingi wa kitaifa wa ulimwengu wa Abeli utapotea. Kwa kutwaa ushindi kunamaanisha kwamba kufanya maendeleo ya kiwango cha dunia ndani ya ulimwengu wa Abeli. Hii ndiyo shughuli yetu ya Kanisa la Nyumbani (Home Church) inayoongoza nyumba 360, kuanzia sasa tutahusika kabisa kati yake. Wale ambao hawana eneo la Kanisa la Nyumbani (Home Church) hawatakuwa na njia ya kufanya ukombozi kwa njia ya malipizi. Kwa kuwa Yesu hakujenga familia yake binafsi,wafuasi wake hawakuweza kubarikiwa katika ndoa au kuanza Kanisa la Nyumbani (Home

Church).
Hata kama mlifanya kazi tangu miaka mitatu katika London au New York, Shetani haitambui ila mkifanya kazi ya Kanisa la Nyumbani ( Home Church). Hata Mungu hawezi kuitambua. Kwa kuwa Mungu alipata msingi wa ushindi, nina uwezo wa kuunda makabila chini ya uongozi wa Kanisa la Nyumbani (Home Church). Tunaweza kuanzisha vita duniani kwa kuongozwa na Kanisa la Nyumbani (Home Church), kwa kuongozwa na makabila. Msingi kama huo uliwekwa. Tunapaswa kushinda Kaini kwa ajili ya kujenga Kanisa la Nyumbani (Home Church) – mtu wa pekee wa aina ya Kaini, na familia aina ya Kaini, ukoo, kabila na taifa. Hatuwezi kurudi nyumbani kwetu bila ya kulipa malipizi na kiwango cha dunia kwa kupitia Kanisa la Nyumbani (Home Church).

Mpaka sasa, wale walioishi maisha ya imani waliacha nyumba zao na kutumikia jamii, kwa kujitolea wenyewe katika kutafuta mbingu kamilifu. Nyinyi pia mliacha nyumba zenu, au sio ? Nilifanya hivyo. Ninajua jinsi gani

Kanuni inakuwa nzuri sana na ya thamani. Basi nilitaka kufundisha Kanuni Takatifu kwa wazazi na kaka na dada zangu kwanza, kabla ya mtu mwingine yoyote. Lakini maongozi ya Mungu sio maongozi ya kuokoa Abeli. Maongozi ya Mungu ni kuokoa Kaini kwa kumtoa mhanga Abeli. Hii ndio sababu vitu vya thamani anapewa Kaini, sio kwa Abeli. Hii ndio Kanuni. Nilitoa maisha yangu yote bila kumuuzia mama mzazi wangu hata kipande cha nguo. Nilifanya mambo mengi mno kwa ajili ya walimwengu; lakini kwa shida tu niliweza kuwafanyia chochote watoto wangu mwenyewe. Tunadhaniwa kurudi nyumbani kwetu baada ya kujenga sharti la Kanisa la Nyumbani (Home Church) na viwango vya mtu binafsi, familia, ukoo, kabila,taifa na dunia. Tuko sasa katika njia ya kurudi.

Abeli anafahamika kwa upendo wake
Mwaka huu nilinunua nguo na zawadi kwa ajili ya Mama na Watoto. Ingawa niliviuza, haiharibu Kanuni. Viongozi wa Japan – je, nyinyi hamfundishi Kanuni ambayo siifundishi, mnaposema, “Mimi ndiye Abeli kwa sababu mimi ni kiongozi wa Kanisa. Nyie ni Kaini. Kaini anatii Abeli. Hii ndiyo Kanuni basi mtii .” Hakuna Kanuni kama hiyo. Mtu ambaye hatimizi kazi yake na kupata kuwa onekano la upendo sio Abeli. Watu kwa kawaida na kwa urahisi wanainama mbele ya nguvu za upendo. Sawa kweli na kiwango cha familia, ukoo au kabila. Basi kama Shirika la Umoja ni Shirika la Abeli na kiwango cha dunia, inapaswa kutwaa ushindi kwa kumwaga damu na kiwango cha dunia, na inapaswa kutwaa sahihi ya Shetani juu ya hati ya kuthibitisha ushindi. Hapo tu ndipo Shirika la Umoja linaweza kuwa Abeli na kiwango cha dunia kwa mara ya kwanza.

Kwa kweli, Hawa anasimama katika nafasi ya Abeli kwa wakati wa ukombozi. Basi kwa miaka mitatu, nyie waume mngetakiwa kufuata kabisa wake zenu. Inaweza kuwa bora kwa kila mmoja wenu kufanya kazi kwa kuwa mbali na mke wako kwa hivyo mnaweza kujiendeleza wenyewe na yeye anaweza

kukuheshimu vile inavyotakiwa mtakapokuja kuwa pamoja. Upito wa miaka mitatu baada ya Baraka ni kipindi cha aina hiyo.

Utamaduni wa Japan ni "copy-cat" ya dunia inayobakia. Kwa hivyo, Japan isingejitunzia vitu yenyewe. Kama haitavitumia kwa ajili ya dunia, Japan itaangamia. Wa-Japan waliojiunga na Kanisa la Umoja wanapaswa kupata kuwa raia wa kimbingu. Raia wa kimbingu ni watu ambao wanaweka upeo wa kimaadili kwa ajili ya watu wote.

Hata kama mmebarikiwa, bado mnapaswa kutimiliza sharti ya malipizi ya kihistoria, kwa kupata mitume watatu halafu 12 na wafuasi 72. Mnapaswa kufikiri sana juu ya yale. Nyie hamstahili kubarikiwa, lakini mimi ninawapatieni Baraka kwa vyovyote. Kwa kuwa Baraka hii ndio nyumba yenu, kama mtainajisi, mtalazimika kuikomboa kwa kunusuru maisha yenu. Ingawa hamstahili kupokea Baraka, mnaweza kurithi kila kitu kama watoto wa Wazazi wa Kweli, kwa sababu mnasimama katika nafasi ya kupata jina lenu juu ya hati za kumiliki. Kwa sababu ya Kanuni hii ya dunia ya kimbingu, Baraka yenu inawezekana. Shindano lenu ni la kupitia mbali milki ya anguko la Adamu na Hawa. Pandeni juu ya mabega ya Wazazi wa Kweli na ruka toka pale kwenda kwa Mungu na watu wote katika dunia ya kiroho watawasaidieni papo hapo. Je mume na mke ni miliki yao wenyewe ? Hapana, wanamilikiwa na Mungu na ulimwengu. Upendo sio wenu. Unamilikiwa na Mungu na jamii ya watu. Basi katika miaka mitatu ijayo, kimbia kwa ajili ya Mungu. Kimbia, kwa kuendeleza roho yenu ya upendo. Unapopenda mke wako, binti wa Mungu, mpende kwa roho ambayo unamuabudia Mungu. Kama upendo wako hauna nguvu za kutosha, Mungu hatasisimuka.

Kama watu wanaokuzunguka hawaangalii familia yenu kuwa stahilifu, ni kwa sababu upendo wenu haujakuwa bado wa kutikisika kwa kutosha. Mke anapompenda mume wake, yeye angempenda kwa roho ambayo anamuabudia Mungu. Kama tendo la kutoa na kupokea la upendo ndani ya familia linaweza kumshtua Mungu, msingi wa nafasi nne umejengwa na familia itanufaika. Kama tunazungusha upesi upande wa juu wa kipuuzi, kwa kushika msumari wa kati wa kusimama, kitazunguka vizuri. Lakini kama tutafanya msumari wa kati geugeu, itayumbayumba. Kwa hivyo kama tunajenga familia kwa upeo wa upendo imara na usiobadilika sio tu watoto wenye afya tele kiroho, lakini wajukuu wa ajabu, wanaoweza kuyakinishwa. Basi kama mnataka kuwa na mtoto mzuri, fanya upande wa juu wa upendo wako imara. Basi kila kitu kitakomeshwa. Mnapaswa kuunda familia ya nafasi nne chini ya uongozi wa upendo kama huu.

Mtu anafanya msingi wa nafasi nne kwa kufikiri juu ya mbingu, watu wote, na mweza wake. Hivi, mbingu, walimwengu, na mume na mke wanakuwa wameungana. Adamu na Hawa walianguka bila kuweka upeo kama huo. Kwa hivyo, kwanza kabisa, tunapaswa kila mmoja kufanya bidii kwa kuweka upeo huu. Lengo letu ni kupenda mbingu na watu wote, tukiendeleza upendo wetu kwa

kujitolea sisi wenyewe.  Tafadhali mkumbuke kwamba

mlibarikiwa kwa kusudi hili. Kama mtafanya hivi, mtakuwa huru kwa shtaki la milki wa anguko.  Huu ni mtazamo wa Kikanuni.  Dunia ya anguko inajiweka yenyewe katikati.  Watu walisahau kuhusu mambo kama upendo wa Mungu, jamii ya binadamu, uzao, vitu vyote, ulimwengu na vinginevyo.  Lakini tuliumbwa kwa kuwaza juu ya vitu hivyo.

Tuna miaka saba kwa kumaliza upeo wa ukamilifu katika hatua ya ukamilifu.  Tunaandaa kwa ajili ya Baraka kwa miaka mitatu na tunapata wafuasi watatu, tukiweka msingi wa malipizi wa kufananishwa na njia ya Yesu.  Hii inakamilisha utume wa kimasihi na kiwango cha kabila.  Kwa hivyo, hatufanyi kazi kwa ajili ya Kanisa la Umoja la Japan, ila kwa ajili ya taifa.  Mimi ninafanya kazi kwa ajili ya dunia.  Mimi niko hatua moja mbele yenu na nilikuwa nikifanya kazi upesi sana kwa kuandaa njia kwa kufanya kazi ya kufanyika ujenzi, ilikuwa kwa kujenga madaraja, na kuweka nyayo ili mweze kufuata.

Shetani alimpevusha Hawa wakati wa anguko.  Lakini wakati wa ukombozi, Hawa anatakiwa kuvutwa juu hadi kiwango cha ukamilifu kwa njia ya Sherehe ya Divai Takatifu.  Maongozi yafuatayo yanatakiwa kutokea kwa kupitia Hawa aliekombolewa. Nyie waume, ambao mlikuwa wa malaika mkuu waliyeanguka.  Kabla ya Sherehe ya Divai Takatifu, mmekuwa wa malaika mkuu aliyekombolewa, lakini bado mnahitaji kurithi uzazi wa damu kama Watoto wa Mungu.  Kabla ya anguko, Adamu alikuwa mtoto mume wa Mungu.  Kwa kukombolewa, yeye anaweza kupata kuwa mtoto wa kulelewa kwa kupandikizwa kwa njia ya mke aliekombolewa, na halafu anaweza mwishoni kuzaa tunda.  Haya ndiyo maarifa yetu.  Kwa kufuata kanuni gani hii inawezekana ? Kwa kuwa malaika mkuu mmoja alianguka kwa kupitia Hawa, yeye anaweza kuumbwa upya kwa njia ya Hawa aliyekombolewa, kwa kushinda tena nafasi asilia yake kwa kupitia kulipa malipizi.

Ni muhimu kuelewa mambo haya kabla ya sisi kuanza sherehe ya maana sana hii.
Tuombe :
Baba wa mbinguni, tuko hapa kwa kuweka msingi wa ushindi kwa ukombozi wa Hawa.  Sisi tunahitaji msingi wa kiroho ambao kwa njia yao tunaweza kukomboa bibi arusi kama mke wa milele.  Ninatamani sana ubariki waume na wake hawa ili waweze kusimama katika nafasi ya watoto ambao wanaweza kuzaliwa upya juu ya msingi wa divai takatifu hii.  Ninaomba uwalinde ili waweze kuzaliwa tena na waweze kufaulu kushinda milki ya ukombozi kwa malipizi na kufuata njia inayoongoza kwa upendo wako katika miaka mitatu ijayo.  Tafadhali walinde.  Naomba kwa shukrani katika jina la Wazazi wa Kweli.  Amina.